*)*

TANGAZO LA SERIKALI NA. la tarehe 17/2/2023

SHERIA YA MIPANGO MIJI,
(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetolewa chini ya kifungu cha 8(1) na 23(1))*

AMRI YA MIPANGO MIJI YA KURASIMISHA MAKAZI YASIYOPANGWA KATIKA ENEO LA MAJENGO YA MWAKA, 2023

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Mipango Miji ya Kurasimisha Makazi yasiyopangwa Eneo la Majengo ya Mwaka, 2023.

Utangazaji wa eneo la upangaji Sura ya 355

2. Eneo lililobainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji (mpango wa urasimishaji) kwa madhumuni ya Sheria ya Mipango miji.

Mpango katika eneo la kwenye Jedwali

3. Mipango ya jumla na kina katika eneo la kwenye Jedwali itaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipango Miji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Newala.

*Tanagazo la seriakali na.77 (linaendelea)*

---

JEDWALI

---

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la upangaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:-

"Unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba M1 yenye majira - nukta 535862MS, 8822382KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Mashariki katika uelekeo wa $70^0$ 12'04'' kwa umbali wa kilomita 0.998 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba M2 yenye majira - nukta 536801MS, 8822720KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Mashariki katika uelekeo wa $14^0$ 19'05'' kwa umbali wa kilomita 0.485 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba M3 yenye majira - nukta 536921MS, 8822250KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Magharibi katika uelekeo wa $66^0$ 52'58'' kwa umbali wa kilomita 0.44 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba M4 yenye majira - nukta 536516MS, 8822077KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini katika uelekeo wa $12^0$ 21'06'' kwa umbali wa kilomita 0.148 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba M5 yenye majira - nukta 536484MS, 8821932KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Magharibi katika uelekeo wa $12^0$ 21'06'' kwa umbali wa kilomita 0.375 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba M6 yenye majira - nukta 536163MS, 8822126KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Magharibi katika uelekeo wa $83^0$ 13'08'' kwa umbali wa kilomita 0.448 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba M7 yenye majira - nukta 535718MS, 8822073KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Mashariki katika uelekeo wa $49^0$ 10'14'' kwa umbali wa kilomita 0.44 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba M8 yenye majira - nukta 535827MS, 8822167KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Magharibi katika uelekeo wa ¼$6^0$ 36'10'' kwa umbali wa kilomita 0.12 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba M9 yenye majira - nukta 535793MS, 8822282KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Mashariki katika uelekeo wa $34^0$ 49'28'' kwa umbali wa kilomita 0.12 hadi ulipoanzia."

Dodoma,
…………, 2023

ANGELINE S. MABULA,
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*